



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA VYAMA VYA SIASA



(Limeundwa chini ya kifungu 21B cha Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa namba 7 ya mwaka 2009)

Simu: +255 22 2137232

Fax: +255 22 2136924

S.L.P 63010,

Dar es Salaam,

20 Juni, 2021.

TAARIFA KWA UMMA.

PONGEZI ZA BARAZA LA VYAMA VYA SIASA KWA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MHESHIMIWA SAMIA SULUHU HASSAN NA RAIS WA ZANZIBAR MHESHIMIWA HUSSEIN ALI MWINYI.

Kamati ya Uongozi ya Baraza la Vyama vya Siasa katika kikao chake cha tarehe **03 Juni, 2021** iliazimia kuwa, kwa niaba ya Baraza la Vyama vya Siasa itoe pongezi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuwa Rais wa Tanzania wa awamu ya sita na Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Hussein Ali Mwinyi kwa ushindi wa kishindo aliopata katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 na kuwa Rais wa Zanzibar wa awamu ya nane.**

Aidha, Kamati ilimpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar kwa kudumisha Demokrasia ya Vyama vingi hapa nchini kwetu kwa kuweka mazingira mazuri ya kufanya Siasa katika pande zote mbili za Muungano wetu na kushirikisha Vyama vya upinzani katika Serikali zao.

Kamati pia ilimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuamua kuonana na Vyama vya Siasa. Hivyo, Kamati kwa niaba ya Vyama vya Siasa vyote vyenye usajili wa kudumu ambavyo kimsingi vyote ni wajumbe wa Baraza la Vyama vya Siasa, iliahidi kushirikiana na Serikali zote mbili, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, katika kuleta maendeleo ya Watanzania. **Pia iliazimia kuwa Vyama vya Siasa vipo tayari kuonana na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa utaratibu na wakati atakaoelekeza kwa kuwa Rais ana majukumu mengi ya kitaifa.**

Wajumbe wa Kamati walimuomba Mwenyezi Mungu aendelee kuwapa afya njema viongozi wetu hawa na ujasiri wa kudumisha Demokrasia ya Vyama vingi vya Siasa, sambamba na kuleta maendeleo zaidi katika pande zote mbili za nchi yetu ya Tanzania.

Mungu Ibariki Afrika, Mungu Ibariki Tanzania, kazi Iendelee.

**John Magalle Shibuda
MWENYEKITI,
BARAZA LA VYAMA VYA SIASA - TANZANIA.
20 Juni, 2021.**